



Uratibu Wa Homa Vijijini Kwa Kutumia Wahudumu Wa Afya Vijijini (CORPS) wilayani Korogwe

Ruta ASM, Sadi JY, Francis F., Malecela EK, Ishengoma DRS, Kamugisha ML., Mmbando BP. na Lemnge M M
Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Kituo cha Tanga, S.L.P 5004 Tanga, Tanzania

Utangulizi

Ugonjwa wa malaria umeendelea kuwa tatizo kubwa nchini na Afrika kwa ujumla. Takwimu zinaonyesha kuwa vifo vingi vya watoto chini ya miaka mitano vinatokana na malaria. Pia mama wawawazito wanafuatia kwa kuathirika. Uchunguzi wa kimaabara wa kugundua vimelea vya malaria mwilini mwa mgonjwa ni tatizo kubwa hasa kwenye sehemu ambazo hazina maabara na wataalamu wake. Ukosefu wa huduma ya maabara na wataalamu husika unachangia sana matumizi holela ya dawa na kusababisha usugu wa dawa husika na vifo visivyo vya lazima. Shirika la Afya Duniani linapendekeza, chini ya Roll Back Malaria (RBM) kutambua homa mapema na kutoa matibabu sahihi ndani ya saa 24 katika sehemu ambazo hazina huduma tajwa hapo juu. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kutumia mbinu ya kutoa huduma ya afya ya msingi vijijini kwa kutumia wahudumu wa afya vijijini. Mpango huu utasaidia kukadiria kiwango cha maambukizi ya malaria ili kuwezesha kupata takwimu zitakazo saidia kuchagua vijiji kwa ajili ya kufanyika majaribio ya chanjo za malaria.

Utaratibu

Kuanzia Januari 2006, wahudumu wa afya ya msingi baada ya kupata mafunzo mafupi, kwa kutumia dodoso maalum walijaza taarifa binafsi za wagonjwa waliokuja kupata matibabu kwa ajili ya homa. Kubaini vimelea vya malaria, mgonjwa alichukuliwa kioo damu (BS) wakati wa matumizi ya dawa ya Sulphadoxine-pyrimethamine (SP) na baadaye pia kipimo cha papo kwa papo (RDT) kipindi ilipoanza kutumiwa dawa mseto (ALu), January, 2007. Wahudumu hao waliongozwa na jedwali maalum kutoa dawa hizo ikiwemo paracetamol. Wagonjwa walishauriwa kwenda kwenye kituo cha afya kama mhadumu aliona huduma ya mgonjwa iko nje ya maelekezo aliyopewa huko nyuma. Dodoso hizo zinakusanywa kila wiki na wataalamu toka Kituo cha utafiti Tanga na kuhakikiwa na daktari wa mradi kabla ya takwimu kuingizwa kwenye tarakirishi na baadaye kufanyiwa uchambuzi. Utafiti huu ulihusisha vijiji vya Kwashemshi, Mng'za, Magundi na Kwamhanya.

Matokeo

Jumla ya matukio 11308 ya homa yaliripotiwa kwa wahudumu wa afya wa vijiji katika kipindi cha Januari 2006 mpaka Desemba 2008. Kati ya hao ni asilimia 26 tu ndio ambao walikuwa na vimelea vya malaria wengi wao wakiwa ni watoto wadogo. Takwimu zinaonyesha kuwa ni watu wachache (zaidi ya asilimia 50) kati ya wale waliokuwa na homa walikutwa na vimelea vya malaria. Kijiji cha Kwashemshi kilionekana kuwa na picha ya wazi zaidi katika kipengele hiki. Takwimu pia zinaonyesha kuwa mwaka 2007 ulikuwa na maambukizi ya malaria kwa wingi kuliko miaka mingine. Maambukizi makubwa haya yanatokana na mvua nyingi zilizonyesha mwaka huo ikilinganishwa na miaka mingine. Uchambuzi zaidi wa takwimu hizi, unaonyesha pia kuwa maambukizi ya vimelea vya malaria kulingana na umri/rika na ukanda wa kilipo kijiji (tambarare au milimani), umri wa miaka 5-9 unaongoza kwa maambukizi na maambukizi ya kiwango cha chini yalionekana kwa watoto chini ya mwaka mmoja.

Hitimisho: Faida za mradi huu kwa jamii hii ni pamoja na kusaidia kupunguza kutoa dawa kiholela bila kuhakikisha kuwepo kwa vimelea vya malaria mwilini, huduma ya bure kwa jamii, kuokoa muda wa kwenda Magunga na kuongeza uhusiano mzuri na wanavijiji kwa tafiti zinazoendelea na zitakazofuatia. Matumizi ya RDT yamepunguza sana matumizi holelala ya dawa
Changamoto: Uendeleu wa kazi hii limekuwa changamoto kubwa baada ya ufadhili wa mradi huu kufikia ukomo.

Shukrani: Tunatoa shukrani kwa wakazi wote wa vijiji husika na viongozi wao, Wizara ya Afya, NIMR na Uongozi wa wilaya kwa kufanikisha kazi hii. Pia tunawashukuru wafuatao kwa msaada wao: C. Msokame, Semdoo T., MD Segeja, HA Msangeni, SH Sembuche, J. Akida, na waingizaji katika tarakirishi, na wokusanyaji wa takwimu. Kazi hii inafadhiliwa na African Malaria Network Trust (AMANET), MalariaGEN na Chuo Kikuu, Oxford. Tulishirikiana pia na Mradi wa DANIDA-ENRECA. Kwa maelezo zaidi wasiliana na: Martha Lemnge; mlemnge@tanga.mimcom.net (027 26 46084).